LEARNING BY EAR - Girls
1st Episode FORCED MARRIAGE.
Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

CHARACTERS:
BIBIY……. Main Character…...Girl, 15 yrs old.
SOFIA…… Girl, 15 Yrs old.
PEER 1…..Girl…14 Yrs.
PEER 2…..Girl….16 Yrs.
OFFICER……Woman ….Adult.
HEAD TEACHER…….Man…Adult.
SOFIAS FATHER…….Man…..Adult.

Intro:
Hujambo na karibu kwenye makala ya jifunze kwa kusikia . makala haya hususan yanalenga maswala mbali mbali yanayo wakabili wasichana . Katika sehemu ya kwanza ya makala haya ya kusisimua tunaangazia ndoa za lazima na pia umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike. Bibiy msichana mrembo na machachari kabisa, anamsaidia rafiki yake ambae anakabiliwa na kitendawili kizito. Je Bibiy atawezaje kukitatua kitendawili hicho?...Karibu kwenye sehemu ya kwanza ya mchezo…Ndoa Ya Lazima katika mfululizo wa makala ya Jifunze kwa Kusikia.

SCENE ONE.
Sign Tune
(Shule inaandaa sherehe ya mwaka .....muziki unasikika kwa mbali, huku wanafunzi wakisika wakiongea. )
MWALIMU MKUU: (apiga kofi mara mbili kuashiria kuwanyamazisha wanafunzi): Kimya tafadhalini…..wanafunzi nasema mnyamae kimya.. (Wanafunzi wanyamaa Kimya) …Asanteni...Naam, kama mnavyojua.. leo ni siku muhimu kabisa katika shule yetu…siku hii ya leo ni siku ambayo mwanafunzi bora katika shule yetu atatunukiwa tuzo ya mwaka. Ni furaha kubwa kwa mwalimu yeyote kusimama mbele ya wanafunzi wake kuzungumzia juu ya mafanikio ya

mmoja ya wanafunzi hao kama leo hii ambapo najiandaa kuzungumzia juu ya mmoja wenu.
(Applause) Na sasa bila ya kupoteza wakati ningependa kumtaja mwanafunzi wetu bora wa mwaka huu ambae ni msichana na kwa kweli amefanikiwa kufikia hapo kwa kuwa yeye ni msichana mwerevu, mwenye adabu njema na juu ya yote yeye ni msichana mwenye bidii .
(Applause)
Na mwanafunzi aliyedhihirisha kufuzu sifa zote hizo nilizozitaja ni,.Sofia(Makofi) Ningetaka Sofia ajitokeze hapa mbele …Sofia…Sofia..tafadhali njoo mbele hapa. .yuko wapi Sofia?

(wanafunzi wananong'ona kwa sauti za chini wanaulizana Sofia yuko wapi?).

PEER 1:Mwalimu mkuu, Sofia hayuko hapa.

MWALIMU MKUU: Sofia hayuko?....kwani yuko wapi?

PEER 2: Hatujui mwalimu mkuu.
(sauti za wanafunzi kwa chini wengine wakisema....labda mgonjwa….kwani yuko wapi..etc.)

MWALIMU MKUU: Wanafunzi hebu nisikilizeni …mmh..Kwa ajili hiyo hatuwezi kuendelea na sherehe zetu, tutalazimika tuahirishe kila kitu hadi wakati mtakapo tangaziwa tena…na kwa sasa sherehe zimevunjika.
(Drums)

SCENE TWO

SOFIA:.....(Analia......)

BIBIY: (Anagonga Dirisha) Hey Sofia! Nifungulie tafadhali.
(Sofia anafungua dirisha na Bibiy anaruka ndani)
What's up Sofie,una nini kwa nini unalia eenh…mbona hukuja shule leo?

SOFIA: Ooooh Bibiy, nina masikitiko makubwa kwa sababu wazazi wangu wanataka niache shule ili niolewe na mzee mmoja tajiri…baba yangu anasema eti elimu haina maana kwa wasichana….ameniambia nijitayarishe kwa ndoa tu…yaani Bibiy mimi hata sijui nifanyeje!

BIBIY: Hapana hiyo haiwezekani!

SOFIA: Lakini huo ndio ukweli mwenzangu na siwezi kufanya lolote kuzuia hilo lisitendeke…Ooh!..mama yangu pia amekubaliana na wazo la baba yangu….kwa kweli Bibiy mimi nimekwisha!!.....nimekwisha!!(Sofia analia tena).

BIBIY: Rafiki yangu Sofia, usiseme huwezi kufanya lolote kubadili hali hii, mimi naamini kuwa hakuna lisilowezekana katika historia ya mwanadamu. Kama David aliweza kumshinda Goliath basi hata nasi tunaweza kutafuta mbinu za kukuokoa kutoka kwenye ndoa hii ya lazima . Elimu ni lazima kwa msichana elimu ni faida kwa wasichana na pia kwa familia nzima. Tukipata elimu bora wasichana pia tunaweza kuwa madaktari, walimu, marubani, wanasheria, mainjinia, wakulima bora hata maafisa wa usalama. Ni elimu na ujuzi ndivyo vinavyo hitajika lakini sio kweli kuwa ni wavulana pekee ndio wanastahilikupata elimu.

SOFIA: Hebu fikiria Bibiy mimi nina umri wa miaka 15 tu sijui hata maana ya ndoa ni nini Ooh kwa nini unyama huu nifanyiwe mie…mbona asiwe msichana mwingine? Jamani kwa nini mimi. (Sofia analia).

BIBIY: Sofia nyamaza rafiki yangu utajiumiza bure kwa kulia mimi naamini kuwa kila swali lazima liwe na jibu…usiogope inakubidi uwe na moyo mgumu.. wacha neinde kwa sasa ili nikafikiri zaidi nini cha kufanya…nitarudi tena wakati mwingine.. unasikia Sofia..wacha kulia rafiki yangu.

SOFIA: (Sofia anamuaga Bibiy).sawa Bibiy nitafurahi sana

kama utanisaidia rafiki yangu maanake nimekwama kabisa yaani siamini kuwa sitarudi tena shule.

MUSIC

SCENE THREE
(Bibiy anapanga mpango wa kumuokoa Sofia......anazungumza na wenzake…)

BIBIY: jamani hivi nyie mnajua kilichomtokea rafiki yetu Sofia? Kwa kweli nikiwa ambia hamtaamini. Wazazi wake wanataka kumuoza kwa mzee mmoja tajiri!!.(Wanashangaa)

PEER 1: Wee umeyajuaje hayo Bibiy?

BIBIY: Mara tu mwalimu mkuu alipovunja sherehe za mwaka mimi nilikwenda moja kwa moja kwa siri hadi kwa akina Sofia hee ilinibidi nirukie dirishani ili niingie chumbani kwa Sofia..wenzangu nilimkuta akilia huku akiwa na huzuni tele yaani amevunjika moyo…basi hadi nilipofanikiwa kumtuliza ndio akaniambia kila kitu…yaani nilijihisi kama dunia imetumbukia pangoni…sijui kwa nini wazazi wengine wanajifikiria zaidi wao binafsi na kupuuza hisia za watoto wao.

PEER 2: Sasa.. Bibiy, unafikiria tutafanyaje ili tumuokoe rafiki yetu?

BIBIY: Ndio maana nimekuja kwenu marafiki zangu ili niwape mpango nilio nao ninahitaji usaidizi wenu kwa hali yoyote ile ili tufanikishe kumuokoa Sofia na iwapo mnakubaliana nami basi tuinue mikono yetu mbinguni na kusema sala yetu ya kawaida.
PEERS & BIBIY:..(wote pamoja)… Pamoja tunasimama,
Pamoja tumeamua,
Pamoja tumepitisha,
Sasa na wakati ujao,
Kuushinda uovu huu,
Wa ndoa za lazima.

Music….
SCENE FOUR

Bibiy na wenziwe watembelea afisi inayoshughulikia maswala ya watoto)
OFFICER: Naam wasichana naweza kuwasaidia vipi?

PEER 2: Je hii ni afisi inayoshughulikia maswala ya watoto?

OFFICER: Ndio.. je? ni jambo gani limewaleta hapa?

PEER 1: Eeh ..huyu hapa ndio kiongozi wetu nadhani yeye atakueleza vyema.

OFFICER: Naona kweli yeye ni kiongozi maanake anaonekana tofauti kabisa na nyie wengine, Loo! Mtindo wa nywele zake unanikumbusha siku zile za mfalme wa muziki wa Reggae, Bob Marley. Kwa kweli anapendeza sana. Nina hakika kwamba huyu ni yule binti maarufu anaeitwa Bibiy. Nimewahi kusikia mengi juu ya visa mbali mbali alivyo vitafutia ufumbuzi pamoja na kisa kile cha chatu mkubwa aliyepambana nae ili kumuokoa mtoto kandoni mwa mto lo! Mtoto Yule maskini angeshambuliwa na nyoka yule mkubwa kama si wewe Bibiy.

BIBIY: Ndio hiyo ni kweli kabisa na hivi sasa najitayarisha kumuua chatu mwingine lakini safari hii sio kando yam to bali ni uovu unaotaka kutimizwa na wazazi wa rafiki yetu.

OFFICER:Je uovu huo ni wa aina gani hebu nifafanulie.

BIBIY: rafiki yetu Sofia hivi karibuni anataka kuozeshwa na wazazi wake…yeye ni msichana wa umri wa miaka 15 tu.... ni mwerevu sana katika masomo na hii ina maana kuwa atalazimika kuacha shule. Swala hili linatukera sana mimi pamoja marafiki zangu hawa ndio maana tumekuja hapa kuleta taarifa hii.

OFFICER: Hiyo ni hatua ya kishujaa mmefanya jambo la

maana sana kuleta taarifa hiyo hapa lazima tuzipige vita ndoa za lazima kwa watoto wetu wa kike ambao wanahitajika kuwepo shuleni ..Bibiy ninajivunia sana ushujaa wako yaani unastahili kila sifa za kuwa kiongozi licha ya kuwa wewe ni msichana mdogo tu…endelea na moyo huo huo na wahimize wasichana wenzako wajitahidi wasitumbukie katika mila zilizo pitwa na wakati ambazo zinaendekezwa na baadhi ya wazazi. Naam sasa niwacheni nilifuatilie swala hili katika ngazi zinazohusika. (Peers…. wanafurahia……)

BIBIY: Asanteni sana wenzangu kwa kazi yenu nzuri..na mapambano yetu ndio kwanza yameanza..sasa tunaelekea moja kwa moja hadi kwa kina Sofia lengo tukambadili nia baba yake!..(Wanaitikia sawa, twendeni, etc.)

Music
BABA SOFIA:Nyinyi watoto hata mkijaribu kunieleza nini hamtafaulu Ng'o kunibadili nia wacha niwaambie tena uamuzi wangu haubadiliki katu na wala hausogei popote kama vile mlima Kilimanjaro.. mnasikia.

BIBIY: Lakini kwa nini usimuache Sofia rafiki yetu aendelee na masomo yake? Yeye ni msichana mwerevu zaidi shuleni sijui kama unajua kuwa umesababisha rafiki yetu Sofia asipokee zawadi yake ya kuwa mwanafunzi bora wa mwaka shuleni…Sofia alikuwa na nafasi nzuri ya kujiunga na shule ya upili.

BABA SOFIA: (Kwa Ukali) Wewe ni nani unaethubutu kuniambia eti mwanangu ataenda shule ya upili kama mvulana eeh… ninavyojua mimi binti yangu ameshapata elimu ya kutosha na sasa yuko tayari kuolewa..lazima Sofia aolewe na mzee mwenzangu aliye tajiri ili nipate fedha..tafadhali hebu niwaonyeshe mlango wa kutokea..tokeni kwenye boma langu!..watoto wadogo mnakuja hapa kunihubiria mimi tokeni haraka.

BIBIY: Hapana mzee usitufukuze haraka hivyo, mbona una wageni wengine ambao wamekutembelea hebu geuka nyuma!

BABA SOFIA: (kwa hasira) Wewe kinyangarakata mwenye nywele kama katani sijui wanakuitaje Bofu Mali au vipi sijui umekaa kama sindano iliyokwama kwenye koo langu..hebu ondokeni nyote sitaki kuwaona ..nendeni…ondokeni!
BIBIY: hata kidogo hatuwezi kwenda popote hadi swala hili litakapo tatuliwa.

MWALIMU MKUU: Na hakika swala hili lazima litatuliwe. Sofia lazima aendelee na masomo yake. Sofia ni msichamna mwerevu sana, na mwenye bidii kabisa katika masomo yake. Ni myama gani aliyekuingia kichwani na kukufanya umtoe mtoto wako shuleni? Hujui kama unamuharibia maisha yake ya usoni? Sofia bado ni msichana mdogo hafai kufunga ndoa hiyo ndiyo sababu iliyotuleta hapa kwako na huyu hapa ni ofisa wa maswala ya watoto.

BABA SOFIA: Hebu nikwambie pia wewe mwalimu mkuu kwanza utambue kuwa hapa ni kwangu na cheo chako hakifanyi kazi hapa..pili umauzi wangu ni wa mwisho na wala haubadiliki..mke wangu na mie tunataka mtoto wetu aolewe ili atuletee utajiri..basi hatutaki jingine.

OFFICER: Baba Sofia, ndoa za lazima ni tatizo ambalo linafungiwa macho na jamii nyingi licha ya kuwepo matatizo chungu nzima katika uzazi na hata maambukizi ya virusi vya HIV na ugonjwa wa UKIMWI, yote haya kwa sababu kwa sababu ya kuwashirikisha watoto walio chini ya umri katika ndoa, hawajakuwa na ufahamu wa kutosha wa kujikinga namatizo ya aina hii.

BABA SOFIA: Mimi sina mpango wa kuelewa yale unayo nieleza kile ninachokijua ni kwamba Sofia ni binti yangu na nina haki nae isitoshe nina haki ya kuamua kile ninacho kiona kuwa ni bora kwa mtoto wangu.
MWALIMU MKUU: Lakini mzee mwenzangu ndoa sio suluhisho

kwa wasichana wadogo. Suluhisho bora ni kuhakikisha wanapata elimu na ujuzi utakao wasaidia kuwafungulia milango katika maisha yao ya baadae.

BABA SOFIA: Jamani inaonyesha kuwa hatuelewani hata kidogo sababu kubwa inayo nifanya nimuoze mwanangu ni kuwa nitapata utajiri ina maana nyie hamtaki nitajirike sio?

OFFICER: Mzee hivi unamuuza mwanao kama vile ng'ombe? Yaani hufikirii hata shida utakazo zipata kwa kumbadili binti yako kwa fedha za mzee tajiri?

BIBIY: Kwa nini unaona pesa ndio muhimu kuliko maisha ya baadae ya rafiki yetu Sofia..mzee mimi nafikiri Sofia akipata elimu atakupa fedha nyingi kuliko zile utakazopokea kutoka kwa huyo mzee tajiri…nakuuliza kipi muhimu kwako fedha au Sofia kupata elimu?

SOFIA'S FATHER: nyamaza...eeh kichwa cha Bofu Mali wee..mimi nawaambia hivi nataka pesa..pesa kwangu ni muhimu kuliko chochote kile..eeh mmesikia?

MWALIMU MKUU: Mimi bado sikubaliani nawe..nakwambia hivi muelimishe mtoto wako wa kike, utakuwa mfano bora kwa jamii. Nina hakika msichana wako Sofia atakupa sifa siku moja tafadhali badili nia ya kutaka kumuoza mwanao na umuache aendelee na masomo yake.

BABA SOFIA: Hata mkinishawishi vipi nawambia Ng'o! sibadili nia na sasa sitaki tena kusikia upuuzi wenu na wala sitaki kumsikia mtoto huyu mwenye kamba kichwani akiniuliza nichague kati ya fedha na elimu ya mwanangu…mimi nasema hivi.. Sofia ataolewa mkitaka mistake tena kwa sababu moja tu muhimu..Pesa… ndio!! Pesa!

BIBIY: Ahaaa! Basi ikiwa pesa ndio chanzo cha rafiki yetu Sofia kuozeshwa hiyo isiwe sababu tunaweza kufanya kitu kumuokoa …Mwalimu mkuu unaonaje tukifanya mchango

shuleni kwetu ili tupate fedha za kumpa Baba Sofia kwa ajili ya kumrudisha rafiki yetu Sofia shule?

MWALIMU MKUU: Oh kweli kabisa hilo ni wazo zuri Bibiy…..mnakumbuka kuna ile michoro na kazi za kufuma mlizotengeneza wakati Fulani tunaweza kuuza vitu hivyo ili tupate fedha.

BIBIY: Ndio na hizo pesa baba Sofia unaweza kuanzisha biashara ndogo..tafadhali nakuomba ufikirie tena juu ya maisha ya Sofia.. rafiki yangu ana miaka 15 tu huoni kwamba anahitaji elimu Sofia ni mwerevu sana darasani.

BABA SOFIA:Sawa basi nitafikiria..hebu nipeni muda kidogo.
BIBIY: Nitafurahi sana kama utabadili nia yako..wenzangu wote na walimu pia tutafurahi kumuona Sofia akirudi shuleni..mimi najua utabadili nia yako.

MWALIMU MKUU: Hata mimi nina imani kuwa wazo hilo la kuchangisha fedha litakutia motisha katika kuliangalia swala zima kwa undani..lakini hii isiwe sababu ya kuwafanya wazazi wengine wawageuze binti zao kuwa ni vitega uchumi kwa ajili ya kupata fedha…baba Sofia hebu jaribu kufikiria tuliyokwambia.

BABA SOFIA: Nimesikiliza yote mliyoyasema na kwa kweli nafikiri wazo lenu sio baya.. linaweza kunisaidia..niwacheni nififikirie wazo hilo kwanza.. ..nawaomba mrudi tena baada ya siku chache. Nina hakika nitakuwa nimepata uamuzi.

Music…

Autro: Na kufikia hapo ndio tumekamilisha sehemu ya kwanza katika makala ya Jifunze kwa kusikia mchezo wa hadithi unaogusia maswala ya wasichana. Ukitaka kusikiliza tena sehemu hii ya kwanza au kumfahamisha rafiki tembelea mtandao wetu, HYPERLINK "http://www.dw-world.de/lbe" www.dw-world.de/lbe Ungana nae tena msichana Bibiy katika sehemu ya pili ambapo anwasaidia wasichana wengine kujenga

ukakamavu. Hadi wakati mwingine kwaheri kutoka kenye makala ya Jifunze kwa Kusikia.

END